HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA

==

MAELEZO MUHIMU KWA WAOMBAJI WA ZABUNI YA UPANGISHAJI WA VYUMBA VYA BIASHARA KATIKA STENDI YA MABASI NYEGEZI

ZABUNI NA. LGA/089/2022-2023/NC/20-26

(FEBRUARY, 2023 HADI JUNI 30, 2023)

Imetayarishwa:
Halmashauri ya Jiji,
S.L.P. 1333,
Mwanza
Simu: +255 28 2501375
Nukushi: +255 28 2500785
Parua Pepe: cd@mwanzacc.go.tz
Tovuti: www.mwanzacc.go.tz

FEBRUARY 2023

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA

Simu: Mkurugenzi: +255 28 2501375

Ofisi Zote: +255 28 40334

Nukushi: +255 28 2500785

Barua Pepe: cd@mwanzacc.go.tz

S.L.P. 1333

MWANZA.

TANGAZO

UPANGISHAJI VYUMBA VYA BIASHARA KATIKA STENDI YA MABASI NYEGEZI MWAKA WA FEDHA 2022-2023

ZABUNI NA. LGA/089/2022-2023/NC/20-27

Mkurugenzi wa Jiji la Mwanza anawatangazia Wananchi wote wanaotaka kupanga Maeneo ya Biashara Katika Stendi ya mabasi Nyegezi iliyopo Halmashauri ya Jiji la Mwanza kwamba wanatakiwa kuomba maeneo hayo kama ifuatavyo: -

A) **MADUKA MZUNGUUKO WA NJE YA STENDI**: 1,2, 3, 4, 5, 6, 7, 8, 9, 10, 11, 12, 13, 14, 15, 16, 17, 18, 19, 20, 21, 22, 23, 24, 25,26,27,28,29,30,31,32,33,

B) **MADUKA YA MZUNGUUKO NDANI YA STENDI: 34,35,36,37,38,39,40,41,42,43,44,45,46,47,48,49,50,51,52,53,54,55,56,57,58,59,60,61,62,63,64,65,66,67,68,69,70,71,72,73,74,75,76,77,78,79,80,81,82,83,**

C) **VYUMBA VYA TIKETI: 01,02,03,04,05,06,07,08,09,10,11,12,13,14,15,16,17,18,19,20,21,22,23,24,25,26,27,28,29,30,31.32.33.34.35.36.37,38.**

D) **MAMA LISHE (RESTAURANT): 001,002,003**

E) **MADUKA MAKUBWA KATIKA JENGO LA UTAWALA: 084,085,086,087,088,090,091,092,093,094,095,096,097,098,099,100,101,102,103,104,105,106,107,108,109,110,111,112,113,114,115,116,117,118,119,120,121,122,123,124,125,126,127,128**

F) **SUPERMARKET: 001**

G) **BANK: 001,002,003,004**

MASHARITI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WA ZABUNI:

i) Ada ya maombi ya zabuni hii ni kama ifuatavyo ambazo hazitarejeshwa;

S/N	ZABUNI NAMBA YA ENEO LA UPANGISHAJI	GHARAMA KWA MITA MOJA YA MRABA/VIWANGO VYA MALIPO	ADA YA ZABUNI
1.	ZABUNI LGA/089/2022-2023/NC/20 Maduka ya mzunguuko wa nje ya stendi	Tsh 27,322.40/=	TSH. 100,000.00
2.	LGA/089/2022-2023/NC/21 Maduka ya mzunguuko wa ndani ya stendi	Tsh 27,322.40/=	TSH. 100,000.00
3			
3.	LGA/089/2022-2023/NC/22 Vyumba vya Tiketi katika Jengo la utawala	Chumba kimoja kitapangishwa kwa Mawakala wanne (4) waliosajiliwa kisheria kufanya kazi hii @ atalipa Tsh 150,000/= kwa mwezi	TSH. 100,000.00
4.	LGA/089/2022-2023/NC/23 Mama lishe (Restaurant)	Tsh 27,322.40/=	TSH. 100,000.00
5.	LGA/089/2022-2023/NC/24 Maduka makubwa katika jengo la Utawala	Tsh 27,322.40/=	TSH. 100,000.00
6	LGA/089/2022-2023/NC/25 Supermarket	Tsh 27,322.40/=	TSH 100,000.00
7	LGA/089/2022-2023/NC/26 Bank	Tsh 40,983.01/=	TSH 100,000.00
8	LGA/089/2022-2023/NC/27 Huduma ya Ubebaji wa mizigo kwa vitoroli katika Stendi	Mwombaji aonyeshe kiwango atakacho kusanya kwa mwezi kwa niaba ya Halmashauri na kiwango anachotaka kulipwa kwa asilimia ya makusanyo	TSH 100,000.00

N.B: Mzabuni atatakiwa kuambatanisha nakala ya risiti ya ada ya maombi
Sheria ya Manunuzi ya Umma namba 7 ya Mwaka 2011 kifungu namba 84(a,b)
Kinakataza kiongozi au Mtumishi wa Jiji kujihusisha na zabuni .

ii) Ada ya maombi uliyolipa ni kwa ajili ya kupata maelekezo ya Zabuni (Tender Document), katika **Tender Document** kuna masharti na vigezo vya nyongeza kwa Zabuni hii. Maelekezo ya zabuni yanapatikana kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni.

iii) Wafanyabiashara wote waliohamishwa kupisha ujenzi watapewa kipaumbele endapo atakua na Ilani, Hadaiwi kodi ya Pango na amekidhi vigezo vyote vya zabuni

iv) Kwa mwombaji aambatanishe Stakabadhi ya malipo ya kodi kuanzia Julai, 2022 hadi Januari 2023; Leseni halali na Hai; Stakabadhi ya Ununuzi wa Zabuni na Namba ya Usajili wa mlipa kodi (TIN/VAT).

v) Tamko dhidi ya vitendo vya Rushwa.

vi) Asiwe Mtengeneza Migogoro na Halmashauri ya Jiji.

vii) Asiombe Zabuni na kupangisha mtu mwingine.

viii) Mikataba yote itadumu kwa kipindi cha miezi minne (4) kuanzia tarehe 1 Machi 2023 hadi tarehe 30 June 2023.

ix) Asiwe msumbufu wa kulipa kodi za Serikali.

x) Maombi yote yafungwe kwa lakiri na bahasha juu iandikwe namba ya Zabuni na kuiwasilisha Ofisi ya Mkurugenzi chumba No. 13 na ziwekwe katika sanduku la Zabuni.

Juu ya bahasha iandikwe fungu unaloomba na itumwe kwa*:*

***KATIBU BODI YA ZABUNI*,**
***HALMASHAURI YA JIJI*,**
***S.L.P 1333*,**
***MWANZA*.**

xi) Mwisho wa kupokea zabuni ni **saa nne (4) kamili asubuhi** (saa ya Afrika Mashariki) ya tarehe **20/02/2023** siku ya Jumatatu katika **Ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji** zilizopo **Halmashauri ya Jiji la Mwanza.** Waombaji au wawakilishi wa waombaji wanaalikwa kushuhudia ufunguzi. Ufunguzi utafanywa mara tu baada ya saa ya mwisho ya kupokea zabuni mbele ya waombaji au wawakilishi wa waombaji waliochagua kuhudhuria ufunguzi huo utakaofanyika katika Ukumbi Mkubwa katika ofisi za Halmashauri ya Jiji la Mwanza

xii) Uongozi haulazimiki kumchagua mzabuni yoyote. Aidha, wazabuni au mpangaji yeyote ambao walipewa vyumba miaka iliyopita na wakashindwa kutekeleza matakwa ya mkataba ikalazimu uvunjaji wa mkataba kati ya Halmashauri na Mzabuni/mpangaji, hawaruhusiwi kuomba zabuni

xiii) Maombi yatakayowasilishwa baada ya muda uliopangwa kuisha hayatapokelewa na hayatafunguliwa.

ERICK MVATI
KNY:MKURUGENZI WA JIJI
MWANZA.

2. MAELEZO YAKINA YA ZABUNI:

i) Utangulizi:

Halmashauri ya Jiji la MMwanza katika jitihada za kutekeleza dhamira yake ya kuwaletea ustawi wa maisha na maendeleo wananchi wa Jiji la Mwanza na watanzania kwa ujumla imekuwa ikitoa fursa sawa kwa wananchi wa jinsia zote kujipatia maeneo ya kufanyia biashara katika Stendi ya mabasi Nyegezi kwa utaratibu wa upangaji ili waweze kufanya biashara, kujipatia kipato na ajira.

ii) Madhumuni ya Upangishaji

Madhumuni ya Zabuni hii ya upangishaji ni kuwezesha umma kupata fursa sawa ya kuwa wapangaji wa Halmashauri ya Jiji kwa Mwaka wa fedha 2022/2023 utakaoanzia 01/03/2023 - 30/06/2023 na Halmashauri kuweza kukusanya Mapato ya kodi ya pango ili iboreshe utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Aidha ni kutekeleza matakwa ya Sheria Na 7 ya Manunuzi ya mwaka 2011, Sheria Ndogo ya Halmashauri ya Jiji la Mwanza (Fees and Charges) ya mwaka 2008 na Mkataba wa upangishaji.

iii) Utaratibu wa Kupata Wazabuni/Wapangaji

Utaratibu wa kupata wapangaji ni wakisheria kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi Namba 7 ya mwaka 2011 kupitia;

- Tangazo la zabuni kwa Umma
- Ufunguzi wa zabuni hii utakuwa siku ya tarehe 17/02/2023, saa 4.00 kamili asubuhi
- Mchakato wa tathimini kupitia kamati ya Tathmini
- Kupewa (award) kupitia bodi ya Zabuni
- Kusaini mikataba ya upangaji

iv) Sifa za Mzabuni (anayeomba kuwa Mpangaji)

Muombaji wa Zabuni hii anatakiwa kukidhi vigezo vyote vya kisheria ikiwa ni pamoja na:-

- Awe mfanyabiashara au anayetaka kufanya biashara hivyo anatafuta eneo rasmi la kufanyia biashara

- Awe ana akili timamu na ana umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea.
- Awe tayari kufuata matakwa ya Sheria na mkataba wa upangishaji na asiwe mpenda Migogoro.
- Asiwe amelimbikiza madeni ya kodi ya pango kwa wapangaji wa zamani kwa anayeomba kuendelea

v) Majukumu ya Halmashauri

Katika mchakato huu wa zabuni majukumu ya Halmashauri ni pamoja na:-

- Kutangaza na kusimamia zoezi la zabuni kwa mwaka wa fedha 2022/2023
- Kupitia maombi yote (kufanya tathmini) ya waombaji na kupata wapangaji wanaokidhi vigezo.
- Kutengeneza mkataba wa makubaliano kati ya mpangaji na mmiliki (Halmashauri ya Jiji)

vi) Utaratibu utakaotumika kufanya malipo

Malipo yeyote ya Serikali yatafanywa kwa njia ya Benki au mifumo ya benki au mifumo ya kompyuta na si vinginevyo. Ada ya Zabuni italipwa Benki kwa mkupuo mmoja na haitarudishwa iwapo utakosa Zabuni hii. Kodi ya pango kwa wale watakaopata Zabuni watalipa kwa mkupuo mmoja kwa miezi minne kabla ya kusaini mkataba .

Vii) Tamko dhidi yaVitendo vya Rushwa

Muombaji wa Zabuni anapaswa kujaza na kusaini fomu maalum ya tamko la kupinga vitendo vya rushwa kwani ni kinyume cha Sheria na haki za msingi.

NB: Kila Mpangaji/Mzabuni anapaswa kuonyesha ni eneo gani anaomba kwenye maombi yake ya zabuni ya upangishaji wa maeneo mbalimbali ya biashara **(Jaza kwenye fomu ya taarifa/Maelezo binafsi ya Mzabuni Mpangaji)**

HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA

MAELEZO/TAARIFA ZA MZABUNI

UPANGISHAJI WA MAENEO MBALIMBALI YA BIASHARA KWA MWAKA 2022/2023
ZABUNI NAMBA LGA /089/2022-2023/NC/20-26

1. **JINA LA MWOMBAJI** _____
2. **TAARIFA ZA MAWASILIANO**:
   (a) Anuani _____
   (b) Simu _____
   (c) Simu ya Mkononi _____
   (d) Namba ya Fax: _____
   (e) Barua Pepe _____
   (f) Mahali Ofisi zilipo _____
3. **NINAOMBA ZABUNI YA:**
   (a) Upangishaji wa maeneo ya _____
   (b) Ambayo ni zabuni Namba _____
4. **WADHAMINI:**
   (i) Jina_____Saini_____Anuani_____
   (ii) Jina_____Saini_____Anuani_____
5. **ORODHA YA VIAMBATANISHO:**
   (1) Stakabadhi ya ununuzi wa zabuni
   (2) Leseni ya biashara
   (3) Usajili wa mlipa kodi (TIN, VAT)
   (4) Nakala (Copy) za risiti ya malipo ya kodi ya mwaka (Julai, 2021– Juni, 2022)
6. **UTHIBITISHO:** Nathibitisha kwamba maelezo niliyoyatoa kwenye Nyaraka hii ya Zabuni (Tender Document) pamoja na yale yaliyomo kwenye viambatanisho vyake ni sahihi na kweli.

_____ _____ _____
JINA SAHIHI TAREHE

AHADI YA MTOA HUDUMA KUHUSU SERA DHIDI YA RUSHWA, KANUNI ZA MAADILI NA PROGRAMU YA UKUBALIFU

Sisi_____ [*Ingiza jina la Mzabuni/ Mwombaji*] tunaweka umuhimu katika zabuni ya ushindani unaofanyika kwa misingi ya haki na huru na isiyoruhusu ukiukwaji wa taratibu na kanuni. Tunapenda kuthibitisha kuwa hatutatoa wala kuwezesha moja kwa moja au siyo moja kwa moja ushawishi usiofaa au zawadi kwa ofisa yeyote wa umma, ndugu zake au watu wenye uhusiano wa kibiashara, kuhusiana na kotesheni hii au baadaye katika utekelezaji wa mkataba kama tutafanikiwa.

Tunayo Sera Dhidi ya Rushwa /Kanuni za Maadili na Programu ya ukubalifu inayojumuisha hatua zote muhimu na za kutosha kuhakikisha kuwa ahadi yetu ya kutotoa rushwa iliyotolewa katika maelezo haya itazingatiwa na menejimenti yetu na waajiriwa na pia watu wengine wote wanaofanya kazi nasi katika miradi ya sekta ya umma au mkataba ikiwa ni pamoja na wakala, washauri, wabia wetu, wakandarasi wasaidizi na watoa huduma wetu. Nakala zetu za Sera Dhidi ya Rushwa /Kanuni za Maadili na Programu ya ukubalifu zimeambatishwa.

_____ _____

(Jina la mtu aliyepewa mamlaka) *Sahihi*

_____

Tarehe

_____

Muhuri/ Alama ya Kampuni